TRUTH CENTERED TRANSFORMATION

MODULE 3

KUELEWA UKWELI WA MUNGU & UWONGO WA SHETANI

MWONGOZI WA MWALIMU

Truth Centered Transformation is a ministry of Reconciled World. Learn more at TCTProgram.org

Reconciled World

Yaliyomo

Somo 1: Je tunabadilika?.....1
Utangulizi.....1
Sheria ya Mungu.....3
Review Moduli 1.....3
Mageuzi nchini Fiji.....4
Moduli 1 na 2.....7
Tafakari.....7

Somo 2: Tuwe watumishi wa uumbaji.....8
Utangalizi 8
Hadithi.....9
Somo ya biblia.....10
Uhusiano sahihi na uumbaji.....11

Somo 3: Tunaweza kubadilisha future.....13
Leta utofauti.....13
Kuwa mtu wa kuleta mabadiliko.....14
Hitimisho 18
Kuweka katika vitendo.....19

Somo 4: Mungu ametupa vingi sana.....20
Utangulizi.....20
Somo ya Biblia.....20
Kushinda visingizio.....21
Tunahitaji kuanza kuona yote Mungu aliyotujalia.....22
Wakulima 22

Somo 5: Shetani ni mwongo.....24
Utangulizi.....24
Shetani anasema uwongo gani?.....24
Nini matokeo ya uwongo huu? 26
Tunaondoaje uwongo huu?.....27

Somo 6: Ukadiriaji wa mahitaji.....28
Utangulizi.....28
Familia.....28
Jamii.....29
Kupaumbelesha miradi.....30

Somo 1: Tunabadilika?

Malengo Makuu

1. Kuelewa kama Wakristo Maisha yetu lazima yabadilike kadri tunavyoishi katika kumtii Mungu.
2. Chukua muda kutathmini kama tunatekeleza kwa vitenda yale tunayojua kuhusu sheria ya Mungu katika Maisha yetu na kama tunaona mabadiliko.

Nyenzo zinazohitajika

1. Jozi ya vionyesho — Kadi za filmu za Fiji
2. Karatasi za manila na penseli za rangi

Utangulizi

Soma hadithi zifuatazo

Hadithi 1: Rwanda

Rwanda ni nchi ndogo yenye watu milioni 8.2.
Miaka 100 iliyopita hakukuwa na wakristu lakini hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 kulikuwa na makanisa kila mahali: asilimia themanini na tano ya watu wote nchini Rwanda walikuwa wakristu. Ilianza na uamsho ulioenea kote Afrika Mashariki kwenye miaka 1940 na mamilioni wakiokoka. Miaka ya 1991 na 1993 kulikuwa na vita vikubwa vya kiinjili kule na watu wengi waliokoka.

Lakini, Miezi ya Aprili na Mei 1994, mauaji ya kushtua yalilipuka ambapo watu milioni 1 waliuawa na milioni 2 walilazimika kuikimbia Rwanda. Mauaji haya yalikuwa ni matokeo ya uhasama wa kikabila. Yalifanyika uso kwa uso kwa visu, siyo kwa mabomu wala bunduki. Katika nchi yenye 85% wakristu, Wakristu wawili walikutana uso kwa uso na kuuana kwa visu. Hadithi ya mambo mabaya yaliyotokea ilikuwa vigumu kuiamini. Ilikuwa kawaida KUSIKIA habari za wanawake waliobakwa na kuuawa mbele ya watoto wao, ya mama waliolazimishwa kuwazika watoto wao wakiwa hai. Hakuna yeyote duniani angeweza kuamini kwamba makundi mawili ya wakristu wangeweza kuchinjana sana kiasi hicho.

Hadithi 2: USA

Marekani kote unakuta makanisa kila mahali. Unaweza kusikiliza redio ya kikristu au kutazama runinga ya kikristu popote unapokwenda. Kuna shule za kikristu katika jamii nyingi pamoja na vyuo na vyuo vikuu vya kikristu. Kuna vitabu, tovuti, majarida na magazeti ya kikristu yasiyo na mwisho.
Hata hivyo, Marekani watoto milioni 1.5 wanauawa kilamwaka kupitia kutoa mimba. Nusu ya ndoa huishia kwenye talaka. Takwimu hizi siyo kwa wasio wakristu tu. Cha kushangaza, kiasi cha talaka na kutoa minba ni karibu sawa kwa wasio wakristu.

Hadithi 3: Brazil

Kando ya mto Amazon jamii ni masikini sana na wako mbali. Namna pekee ya kuwafikia ni kwa njia ya mtumbwi. Miaka thelathini iliyopita hakukuwa na wakristu katika jamii hizi. Miaka 30 iliyopita wamisionari walikuja maeneo haya kwa mitumbwi na kuhubiri na watu wakaokoka. Wamisionari wangekaa kwa siku chache, wakaanzisha kanisa, na kisha kwenda katika jamii inayofuata. Sasa ukienda huko unaangua kilio

Kwa sababu wanavijiji ni maskini sana. Katika vijiji hivi familia wana kidogo tu cha kula. Namna ojawapo familia kupata pesa ni kuwakodisha mabinti wao kama makahaba wakati wakiwa na umri wa miaka kumi na mbili kumi na tatu. Baba huwaanda mabinti zao kwa ajili watu tajiri zaidi katika jamii yao. Baba wakristu pia hufanya hivyo – kukodisha watoto wao kwa ajili ya pesa.

- Nini kilitokea katika kila moja ya hadithi hizi?
- Hadithi hizi zinashangaza au hapana? Kwa nini zinashangaza?
- Unadhani Mungu anajisikiaji kuhusu hali hizi? Kwa nini?

Hadithi 4: Kijiji cha mlimani

Kulikuwa na Kijiji kidogo milimani. Kilikuwa katika sehemu maskini ya nchi na watu waliishi maisha ya hali ya chini. Hawakuwa hata na chakula cha kutosha. Walitegemea hali ya hewa kuona kila mwaka ungekuwaje — kingekuwepo cha kutosha au wangekumbana na upungufu? Hawakuwa na vyoo vyovyote na waliishi katika makazi ya hali ya chini sana. Hawakuwa watu wasio na furaha na walifanya kazi za kilimo/ mashambani, wakihangaika mwaka hadi mwaka

Miaka thelathini iliyopita wamisionari wa kwanza walifika sehemu hii na waliwambia kuhusu Kristu. Kadri walivyosikiliza na kuelewa walianza kuamini na wengi wakawa wakristu. Wamisionari walisaidia watu katika eneo hilo kujenga makanisa. Watu walihudhuria kanisani. Walifurahi kwa sababu walijua kwamba wakifa wangeenda mbinguni na walitazamia siku hiyo ya ajabu ambapo wangekutana na mwokozi wao

Wamisionari waliondoka eneo hilo na kanisa liliendelea chini ya viongozi wazawa. Miaka thelathini baadaye wamisionari walirudi. Kanisa lilikuwa limeisha kua na watu walikuwa wamejizatiti. Wakikutana pamoja. Lakini, Kijiji kilikuwa vilevile. Watu walikuwa bado masikini na bado walitegemea hali ya hewa kujua kama wangekuwa na njaa au wanagepata chakula cha kutosha mwaka huo. Bado kulikuwa hakuna vyoo katika jamii yao. Kulikuwa na mabadiliko kidogo sana.

- Nini kilitokea katika hadithi hii?
- Je hadithi hii inashangaza? Kwa nini au kwa nini hapana?
- Nini ni kilekile kuhusu hadithi hii na hadithi nyingine?

Kwa namna Fulani hadithi iliyopita haionekani kushtusha kwetu kama hadithi tatu za mwanzo kwa sababu ni ya kawaida. Lakini ni kama hadithi nyingine: Wakati ukristu umewaokoa watu haujabadilisha Maisha yao. Mungu anataka maisha yetu ya tofauti duniani, siyo tu mbinguni.

Sheria za Mungu

Soma Kumb. 30:11-20.

- Mungu anaelezaje sheria zake? Je ni ngumu au rahisi?
- Katika mstari wa 15 nini chaguzi zilizo mbele yetu? Wewe ungependelea nini?
- Nini kinaleta Maisha na baraka? (v.15-16)
- Nini kinaleta kifo na laana? (v.17-18)
- Mungu anataka tuchague nini? (v.19)

Soma Kumb. 28:1-14.

- Nini kinatokea tukitii sheria za Mungu?
- Je ahadi hizi ni kwa Maisha baada ya kufa au kwa Maisha tukiwa hapa duniani?

Somo Kumb.28:15-19.

- Nini hutokea pale tusipotii sheria za Mungu?

Mungu ametengeneza sheria nyingi zinazotwambia namna gani tuishi. Kuna sheria za maadili zinazotawala utu wema. Mfano ni, "usizini." Na kuna sheria za asili au za uumbaji zinazotawala mambo tunayoweza kuona. Kwa mfano, kila siku ina masaa 24, au mmea unahitaji maji kustawi.

Kadri tunavyo mheshimu Mungu tutaona Maisha yetu yakiboreka. Tunahitaji kuelewa sheria au kanuni na tuanze kuzitumia katika Maisha yetu. Kadri tunavyofanya hivyo tutaona Mungu akibariki Maisha yetu.

Review Moduli 1

Angalia bango 3 kutoka Moduli 1, Somo 1.

- Ni mahusiano gani picha hizi zinawakilisha?
- Mungu ana sheria au kanuni kwa kila moja ya maeneo haya? Ni zipi ambazo unaweza kufikiria?

Mungu ana sheria kwa namna gani tuendeshe kila moja ya mahusiano haya. Ametupa kanuni kutusaidia tufanikiwe katika kila moja ya maeneo haya na kurekebisha mahusiano yaliyovunjika. Bila shaka, hazitakuwa timilifu hadi Yesu atakaporudi tena lakini zitaboresha.

Katika mafunzo yaliyopita tulifundisha kuhusu mageuzi. Wakati ule watu walikuwa maskini. Isipokuwa kwa matajiri wamiliki wa ardhi wachache na familia za kifalme, watu walio wengi walikuwa maskini na mara nyingi hawakuwa na chakula.

Karibu miaka 400 iliyopita Mageuzi yalikuja Ulaya kaskazini. Kwa mara ya kwanza watu walianza kujisomea biblia. Hawakusubiri padre awaeleze biblia ilichosema. Walianza kujifunza sheria za asili na maadili ambazo Mungu amejenga katika Ulimwengu wake. Sheria hizi kadri muda ulivyokwenda, zilikuja kuanza kufundishwa zaidi na zaidi katika makanisa na shuleni. Kwa mafundisho haya, watu walianza kubadilika —walianza kuishi Maisha yao kulingana na mawazo haya mapya. Kwa mfano, walielewa kwamba Mungu alituambia tufanye kazi kana kwamba tunamfanyia yeye na si mwanadamu (Efeso 6:7). Walielewa pia kwamba tunahitaji kutoa na kusaidiana.

Kadri walivyobadilika jamii zao nazo pia zilibadilika. Chakula kingi zaidi kilizalishwa na kushirikiana rasilimali kulitokea. Familia na jamii ziliimarishwa na watu wengi zaidi walienda shule na walipata elimu. Taifa baada taifa Ulaya kaskazini lilitoka kwenye umaskini.

Kwa kutii sheria za Mungu mataifa ya ulaya yalikuwa matajiri zaidi. Kukana sheria za Mungu hutengeneza umaskini. Kama tunataka kutoka kwenye umaskini tunahitaji kuanza kuelewa kanuni hizi na kuziweka katika vitendo.

Tumepewa Biblia ambayo inaeleza sheria zote za Mungu. Tunahitaji kuzitumia katika kila eneo la Maisha yetu. Haitoshi tu kuja kanisani Jumapili. Mungu anatutaka tumtii muda wote. Tunapofanya hivyo tutaona Maisha yetu yakiboreka. Hiyo haimaanishi kwamba Maisha yetu yatakuwa rahisi. Tukiangalia Maisha ya Paulo tutaona kwamba mara nyingi alikumbana na magumu. Lakini Mungu ameahidi kutubariki tukienenda katika kumtii Yeye. Hata Paulo aliridhika na kupata furaha katika changamoto alizokumbana nazo.

Mageuzi katika Fiji

Maelekezo: Tumia kadi za filamu kueleza hadithi ifuatayo kuhusu Fiji.
Wanafunzi wanaposikiliza hadithi waombe wajiandae kujibu maswali yafuatayo:

1. Namna gani watu walianza kumtii Mungu?
2. Namna gani walianza kuona Mungu akiwabariki?

Kadi za picha za Fiji

1. Utangulizi	Fiji inatengenzwa na visiwa 322. Ni sehemu nzuri ya utalii ambapo watu wengi maarufu huja wakati wa likizo. Mapato makubwa yanatokana na watalii. Kuna watu 850,000 wanaoishi Fiji. Nusu ya watu ni wafiji na nusu nyingine ni wahindi.
2. Matatizo Yaliyo wakumba	Mwezi wa tano mwaka 2000 serikali ilipinduliwa na watumishi wa serikali waliwekwa mateka kwa siku 56 , wakiwa hawawezi kutoroka. Mitaani kulikuwa vurugu na watu walikuwa wakiuana. Maaskari walishambuliana. Hata baada wa watumishi wa serikalai kuachiwa huru bado nchi ilikuwa kwenye hali ya vurugu. Watalii waliacha kuja kwa hiyo watu hawakupata watalii wa kuwauzia vitu.
3. Makanisa kuungana	Makanisa nchini Fiji hayakufanya kazi pamoja wala hayakusaidiana. Badala yake yalishindana. Lakini sasa yalielewa kwamba yanahitaji kuja pamoja na kuomba kwa ajili ya nchi yao. Walipoandaa mkutano wa kwanza hawakujua kama mtu yeyote angehudhuria lakini ukumbi ulifurika viongozi wa makanisa. Walianzisha ushirikiano mpya: Umoja wa makanisa ya kikristo. Wachungaji walisema mwanzoni walijifikiria wenyewe tu lakini sasa walijua kwamba kama wanataka Mungu abariki taifa lao ilikuwa lazima wafanye kazi pamoja.
4. Waziri mkuu wa muda akiri	Mwezi wa saba mwaka 2001 wakristo kutoka nchi nzima waliungana pamoja kwa sala ya pamoja na mafundisho ya biblia. Mwishowe Waziri mkuu wa muda alisali na kumwomba Mungu amsamehe na amwongoze ili aweze kumheshimu Mungu. Muda mfupi baada ya hapo alikuwa Waziri mkuu wa Fiji na aliwatafuta watu wengine wanaomcha Mungu wafanye kazi naye.
5. Zama za giza	Zamani Fiji ilijulikana kwa uchawi na ulaji nyama za watu. Waliweza hata kuwafanya wahanga wakate kuni kwa ajili ya kuchoma miili yao wenyewe. Viongozi wa wachawi wangeweza kutembea juu ya mawe ya moto na wasiungue. Lakini zama hizi ziliacha laana kwenye vijiji. Watu walikufa kimiujiza na haikujulikana kwa nini.

6. Hadithi ya Kijiji kimoja	Kijiji kimoja kilikuwa maarufu kwa ulimaji wa madawa ya kulevya. Mmoja wa marafiki wa kiongozi wa wauza madawa aliugua. Aliogopa kwamba angekufa. Walisikia kuhusu kanisa wakampeleka ili akaombewe. Alipokea uponyaji akampa Yesu Maisha yake. Watu wengine kijijini waliposikia kilichokuwa kimetokea nao pia walimfuata Yesu. Watu walianza kuelewa kwamba walikuwa wamedanganywa na shetani. Waliacha mambo yote ya ushirikina katika eneo lao. Hata muuza madawa ya kulevya naye aliokoka na akaacha kuuza madawa ya kulevya. Sasa 80-90% ya wanakijiji walikuwa wakristu. Viongozi wa Kijiji walifurahi lakini ilikuwa haitoshi. Walianza kukutana kusali pamoja saa kumi alfajiri. Waliomba msamaha na kumwomba Mungu aiponye jamii yao. Sasa watu waliokuwa wagonjwa kila mara hawakuwa wagonjwa tena, Miti ambayo haikutoa matunda ilianza kutoa matunda na bahari ilianza kujaa samaki wakati zamani walikuwemo wachache tu.
7. Mageuzi katika magereza	Watu waliojaribu kupindua serikali walitupwa gerezani. Magereza yalikuwa mahali pasipo na matumaini. Lakini makanisa yalianza kwenda magerezani. Mwanzoni ilikuwa vigumu. Watu walikuwa na chuki kubwa dhidi ya magereza, na walitamani sana kisasi. Hawakuwa tayari kusamehe. Lakini Mungu aliinuka na wafungwa wakawa wakristo. Sasa unaweza kusikia watu wakiimba nyimbo za kumwabudu Mungu gerezani. Ukipita karibu na gereza linasikika kama vile ni kanisa.
8. Mabadiliko zaidi	Mjini pia kulikuwa na mabadiliko mengi. Makanisa yalikutana mara kwa mara kuomba kwa ajili ya miji yao. Walitubu na kuomba msamaha kwa ajili yale waliyotendeana siku za nyuma. Miji ilianza kubadilika. Zamani watu wasingetabasamu lakini sasa walitabasamu. Sasa kuna upungufu katika uhalifu, umaskini, ombaomba na watoto wa mitaani. Watoto wanahudhuria shule. Uchumi unaboreka na watalii wanarejea.
9. Hadithi ya Kijiji kingine	Katika sehemu nyingine hakukuwa na samaki zozote kwa miaka 55 kwa sababu sumu ilikuwa imeharibu maji. Pembezoni mwa mto hakukuwa na mazao. Kila mmoja kijijini alikusanyika wakatubu kwa ajili ya dhambi za mababu zao na kuungama kuacha uchawi. Waliomba Mungu awasamehe. Kwa siku nyingi walikwenda mbele za Mungu na kulia. Kila mtu alileta vifaa vya kichawi na kuviharibu. Matokeo yake Mungu aliponya maji yao na yalijaa samaki. Ardhi karibu na mto iliponywa pia na ilianza kutoa mazao mengi.

Soma pamoja 2 Nyakati 7:14.

- Kwa namna gani walimrudia Mungu?
- Kwa namna gani Mungu aliponya ardhi?

Ni namna gani walianza kumtii Mungu?

- Makanisa yalifanya kazi pamoja
- Makanisa yalianza kusali pamoja
- Watu waliomba msamaha kwa mambo waliyofanya zamani
- Waliacha mambo yanayohusiana na uchawi

Namna gani Mungu aliwabariki?

- Nchi ilistawisha mimea ambapo kabla haiukustawi
- Bahari ilikuwa na samaki
- Chakula cha bahari kilikuwa kingi kuliko awali
- Uhalifu ulipungua
- Watoto wa mitaani walipungua
- Watu walitabasamu
- Watalii walirudi
- Uchumi uliboreka

Kwenye vipindi vijavyo tutaangalia zaidi kuhusu sheria za Mungu. Halafu tutaangalia jinsi shetani anavyotudanganya na kutufunga kwenye umaskini.

Moduli 1 na 2

Tayari tumeisha jadili kuhusu baadhi ya sheria za Mungu katika mafunzo mawili yaliyopita.

KATIKA VIKUNDI VIDOGO

Chini ya kila kichwa cha habari, jaribu kukumbuka ulichojifunza kuhusu mada hiyo. Ama chora picha au fikiria hadithi au mfano wa kila moja ya mawazo haya.

- Mpende jirani yako
- Utoaji
- Kazi
- Kiroho, Kimwili, Kijamii na kiakili

Washirikishe matangazo wanafunzi wengine wa darasa.

Tafakari

Chukua muda kufikiria kuhusu kila moja ya maeneo haya. Unafanyaje kutekeleza mambo hayo? Kitu gani kingine ungeweza kuwa unakifanya?

Somo 2: Twatakiwa kuwa watumishi wa uumbaji

Malengo

1. Kuelewa tunatakiwa kutumika na kutawala uumbaji siyo kutumia vibaya na kutawaliwa na uumbaji.
2. Kufikiria namna ambavyo wamekuwa wakitawaliwa na uumbaji na jinsi ya kuzuia.
3. Kufikiria namna ambavyo wamekuwa watumishi wabaya wa uumbaji na namna ya kurekebisha.

Orodha ya zana

1. Bunda la Vionyeshi — Kadi za uumbaji
2. Begi la maji
3. Nguo ya kusafisha maji
4. Karatasi kubwa ya kuandika mpango

Utangulizi

Weka begi la maji kwenye chumba mahali ambapo halitaharibu kitu chochote likianza kutoa maji lakini ambapo wanafunzi wataliona. Toboa tundu dogo la sindano kwenye begi na uache maji yakiendelea kutoka unapoanza kipindi. Hakikisha tundu ni kubwa la kutosha kiasi cha kufanya maji yatoke haraka kiasi cha kutosha kufanya wanafunzi waone. Anza kipindi na kamilisha mfano huu wakati mtu akiona maji.

Mtu akisema chochote kuhusu maji yanayovuja kutoka kwenye begi mwambie huwezi kufanya chochote kuyazuia. Waruhusu wanafunzi watoe mapendekezo ya kitu gani kifanyike. Kama hakuna yeyote anayetoa mapendekezo basi waulize, “kuna chochote mnaweza kufanya?”

JADILI KAMA KIKUNDI KIKUBWA

- Nini kimetokea?
- Nini kingetokea kama nisingezuia maji yasiendelee kuvuja?
- Ulifikiria nini niliposema “nisingeweza kufanya chochote” kuzuia maji yasiendelee kuvuja?

Mungu anatuambia katika sura ya mwanzo kabisa ya Biblia kuwa mtawala— au kuwa “bosi”—wa uumbaji Wake. Katika somo hili tutaangalia sentensi hii kwa undani zaidi.

Hadithi

Maelekezo: Lisomee darasa hadithi ifuatayo

Wahindi wa kabila la Pokomchi ni kati ya watu maskini kabisa katika jimbo maskini kabisa nchini Guatemala. Miaka thelathini iliyopita, wamisionari walikuja kutangaza injili na kupanda makanisa. Wapokomchi wengi wakamkubali Kristu, lakini jamii zikabaki maskini muno. Wakristu wapya walipata matumaini kwa siku zijazo, lakini si matumaini kwa leo. Kwa kweli, walisubiri kufa ili waache Maisha ya taabu hapa duniani na waende kukaa na Yesu mbinguni.

Hali hii ilibadilika wakati mchungaji kijana, Arturo, alipoanza kufanya kazi kati ya wapokomchi. Alianza kufanya kazi na wachungaji wa kipokomchi wasiojua kusoma na kuandika. Kwa uangalifu aliwafundisha Biblia. Waliposoma aliwaeleza jinsi Mungu anavyotutaka tutumie kanuni na sheria zilizomo kwenye Biblia yake katika Maisha yetu ya kila siku.

Tatizo la kawaida kati ya wapokomchi lilikuwa ukosefu wa maghala ya kuhifadhia mavuno yao. Mara nyingi, wakulima walivuna mavuno mazuri, na kuliwa na panya kabla watoto wa wapokomchi hawajayala. Arturo aliwauliza wakulima, “Nani ni mjanja zaidi, nyinyi au panya?” Wakulima walicheka na kusema, “panya.” Arturo aliuliza, “Mnawatawala panya, au panya wanatawala Maisha yenu?” Wakulima walikubali kwamba panya wanawatawala na familia zao. Walichukua chakula na hakuna aliyewazuia. Panya na si binadamu waliamua nini kingeweza kuliwa.



Kisha, Arturo aliwaonyesha kwamba Biblia imesema kwamba wanaume na wanawake wote waliumbwa. Aliwakumbusha Mungu aliwajalia ubunifu kwa sababu wameumbwa kwa sura yake. Walitakiwa kutumia ubunifu Mungu aliowapa kutii kanuni za kutawala viumbe vyote, na si kuacha viumbe viwatawale

Wapokomchi waliamua walihitaji kutenda kulingana na Biblia na kuanza kutawala panya. Walijenga maghala ambayo yaliwaacha panya nje ya chakula chao. Baada ya chakula kuhifadhiwa dhidi ya panya walianza kuwa na chakula cha kutosha kwa ajili ya familia zao.

JADILI KAMA KIKUNDI KIKUBWA

- Nini kilitokea kwenye hadithi hii?
- Tunaweza kujifunza nini kwenye hadithi hii? Inahusianaje na hali halisi katika eneo letu?

Somo la Biblia

Soma Mwanzo 1:26-28; Mwa 2:15, Zaburi 24:1.

- Dunia ni mali ya nani? (Zaburi 24)
- Mungu alimwambia nini mwanadamu kuhusu uumbaji?
    - *Utawale*
    - *ufanyie kazi*
    - *Utunze*

- Kuutunza maana yake nini? Huwa tunafanya nini tunapotunza kitu? Tunawezaje kutunza uumbaji wa Mungu?
    - *Tunapotunza kitu hukilinda na kuhakikisha hakivunjiki wala kuharibika. Tunaweza kufanya hivi kwa kutochafua au kuruhusu uumbaji uharibiwe. Tunahitaji kuwa waangalifu kuhusu watu kukata miti mingi, kitu ambacho kinaweza kusababisha maporomoko ya ardhi.*
- Kuufanyia kazi maana yake nini? Tunawezaje kufanya hivyo?
    - *Tunapoufanyia kazi tunaufanya uzae kitu. Uumbaji utupatie chakula na uzuri na tupate mahitaji mengine, kwa mfano, vifaa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Tunapofanya kilimo tunafanya Mungu alichotuamuru tufanye. Tujisikie furaha tunapolima kwa sababu tunatii amri hii.*
- Kutawala uumbaji maana yake nini (Fikiria kuhusu hadithi ya Wapokomchi)
    - *Kutawala maana yake tuna udhibiti juu ya kitu. Kwa mfano wa begi la maji, tunaweza kudhibiti mtiririko wa maji— hauwezi kutudhibiti. Tunahitaji kutumia ubunifu wetu kutawala uumbaji. Kwa mfano, daraja hutawala uumbaji. Bila daraja mto huongoza wapi tunaweza kwenda. Kukiwa na daraja au mtumbwi tunaweza kuamua wapi tunataka kwenda. Si mapenzi ya Mungu kwamba tujisikie tunatawaliwa na uumbaji. Tunahitaji kumwomba Mungu atupe njia za ubunifu kutawala uumbaji.*

Tunapotawala, fanya kazi na kutunza uumbaji tunatii amri za Mungu kwetu. Huku tunakuita kuwa na uhusiano sahihi na uumbaji. Bahati mbaya, kwa sababu ya anguko hii imekuwa ngumu zaidi ya ilivyokuwa Mungu alipotoa amri hizi lakini bado Anatutaka tuzitii

Uhusiano sahihi na uumbaji

KIKUNDI KIDOGO CHA - WATU 2-3

Wape kila kikundi seti ya kadi za uumbaji kutoka kwenye bunda la vionyeshi. Waombe watazame kila kadi za picha. Ziweke katika mafungu kulingana na kama zinaonyesha uhusiano sahihi na uumbaji au la.

Wape darasa kadi tupu. Waombe wachore mifano zaidi kila mmoja kutoka kwenye jamii yake.

Wakishamaliza kufanya kazi katika makundi pitia kila kadi. Kwa kila kadi waulize kama huw tunafanya hivi katika jamii yetu. Kwa kadi nzuri waulize kama tunatakiwa kufanya hivi (zaidi); kwa zile mbaya waulize kama tunatakiwa kuacha kufanya hivi. Je tunawezaje kufanya mabadiliko haya?

Waombe darasa wachague mawazo machache na fikiri kama unaweza kufanya haya kama matendo ya upendo.

Kadi za uumbaji

Utunzaji wanyama 	**Maji safi**	**Ustawishaji chakula**
☺ Tumeambiwa kutunza wanyama. Tunahitaji kuwapa banda linalofaa ili wasilete magonjwa katika nyumba zetu. Hii ni namna ya kutawala uumbaji.	☺ Kutengeneza visima na kutumia chujio, kuchemsha maji au kuyaacha juani (SODIS) husaidia kufanya maji yawe salama kwa miili yetu ili yasituuguze.	☺ Tunahitaji kustawisha chakula kwa mahitaji yetu. Hii ni sehemu ya kufanyia kazi ardhi. Bustani ya jiko ni namna nzuri ya familia kupata chakula bora.
Kilimo	**Kujenga nyumba** 	**Choo**
☺ Tunahitaji kulima ardhi Mungu aliyotujalia. Izalishe kwa ajili ya familia yetu, na siyo kututawala. Tunahitaji kuweka njia za umwagiliaji na njia za kurutubisha udongo ili uweze kuzalisha zaidi.	☺ Tunahitaji kibanda kutukinga dhidi ya jua na mvua. Kuhakikisha kwamba tuna nyumba salama ni sehemu ya kutawala uumbaji. Hatutawaliwi tena na jua na mvua.	☺ Choo hupunguza maradhi na huweka mazingira yetu salama. Tunahitaji kutunza mazingira yetu na kuhakikisha hayatusababishii magonjwa.
Uvuvi	**Ukataji miti**	**Mitego ya panya** 
☺ Uvuvi ni namna nyingine tunaweza kupata chakula kwa familia zetu.	☹ Tunahitaji kuwa waangalifu kwamba tunapokata miti tunapanda miti mipya. Miti ni zawadi kutoka kwa Mungu ambayo inazuia maporomoko ya ardhi. Kama tukikata miti na hatuitumii ardhi haraka inaharibika inakuwa haifai kuzalisha chochote.	☺ Mitego ya panya hutusaidia kupunguza panya wanaokula chakula chetu. Mitego ya panya haihitaji kuwa ya kitaalamu sana. Inaweza kutengenezwa kutoka kwenye miti ya mianzi kama mitego hii. Tunahitaji kutawala uumbaji na sio kuacha panya watutatwale watufanye wagonjwa.

Mtego wa Nzi 	**Funika chakula dhidi ya nzi** 	**Kulala ndani ya chandarua**
☺ Mitego ya nzi ni namna nyingine ya kupunguza nzi Tunaambiwa kutawala uumbaji na kupunguza idadi ya nzi ni njia ya kufanya hivyo.	☺ Tunahitaji kukinga familia zetu dhidi ya magonjwa yanayosambazwa na nzi kwa kufunika chakula chetu.	☺ Kulala ndani ya chandarua hutusaidia kuhakikisha hatupati Maleria au mangonjwa mengine yanayosambazwa na mbu.
Takataka 	**Kame/ Ardhi isiyotumika** 	**Kuchimba kisima** 
☹ Mungu alitutaka tutunze mazingira. Hii inamaanisha tuyaweke mazuri ili yamheshimu. Tusitupe takataka chini lakini tuzitupe kwenye vyombo cha takataka.	☹ Tunahitaji kutafuta namna ya kurejesha ardhi isiyo weza kutoa mazao irudi kwenye hali yake ya awali ya kuweza kutoa mazao kwa kutumia mbinu kama umwagiliaji na urutubishaji wa asili.	☺ Visima ni namna ya kupata maji Mungu aliyotuwekea chini ya ardhi. Maji ya visima hutusaidia kukaa wasafi na wenye afya.
Kulima mbogamboga 	**Wanyama nyumbani** 	**Panya kula chakula**
☺ Ulimaji wa mbogamboga ni namna nyingine tunaweza kulisha familia zetu.	☹ Wanyama wasiwe karibu na chakula chetu. Wanabeba magonjwa. Tunatakiwa kudhibiti mifugo yetu na kuwatengenezea mabanda yao.	☹ Panya hueneza ugonjwa na hula chakula tunachohitaji. Tunahitaji kuhifadhi chakula chetu dhidi ya panya na kutumia vitu kama mitego kupunguza idadi ya panya katika maeneo yetu.

Somo 3: Tunaweza kubadilisha siku zetu zijazo

Malengo

1. Kuelewa Mungu hakukusudia tusibadilike. Ana kusudi na miasha yetu na anataka tukue na Maisha yetu yaboreke.
2. Kuelewa jinsi tunavyoweza kuwa watu wanaoleta mabadiliko kwa wengine.

Vifaa

1. Bunda la vionyeshi — Picha ya Familia —Taabu
2. Bunda la vionyeshi —Kadi za picha za Yesu na msiba
3. Bunda la vionyeshi — Kadi za picha kwa Mrs. Lee
4. handouts za wanafunzi

Utangulizi

Maelekezo: Onyesha picha ya Familia — Taabu na uliza darasa:

- Unafikiri familia hii imebadilika katika miezi 6 iliyopita?
- Unafikiri familia hii imebadilika katika mwaka mmoja uliopita?
- Unafikiri familia hii itabadilika baada ya mwezi ujao?
- Unafikiri familia hii itabadilika baada ya miezi sita ijayo?
- Unafikiri familia hii itabadilika baada ya mwaka mmoja ujao?



Kama wakijibu HAPANA kwa maswali yote waulize kwa nini? Kama wakijibu NDIYO waulize mabadiliko haya yatafanyikaje?

Soma tena haya katika somo la kwanza – Kumb 28:1-14.

- Ni kwa namna gani Mungu anataka kutubariki?
- Je haya hizi zinahusianaje na familia hii?

Soma Yeremia 29:11.

- Ni mipango gani Mungu aliyonayo kwa Maisha yetu?
- Je haya hizi zinahusianaje na familia hii? Kwa nini au kwa nini hapana?

KATIA VIKUNDI VIDOGO

Chora picha nyingine ya familia hii kama Mungu alivyokusudia wawe.

Kutengeneza utofauti

"Mtoto wa mfalme atakuwa mfalme, mtoto wa sufii atakuwa sufii."
"Mito ina mida inapokuwa miembamba na wakati inapokuwa mipana, vivyo hivyo pia Maisha ya watu."
"Kupata chakula cha kutosha ni vigumu, lakini kuwa Tajiri ni rahisi."

Angalia: *hapo juu ni misemo ya kawaida – utataka kuchagua misemo ambayo ni muafaka kwa mazingira yako.*

- Nini maana ya misemo hii?
- Unajua msemo mwingine wenye maana sawa?
- Upi kati ya misemo hii unakubaliana nao?
- Upi kati ya misemo hii, kama upo, ni sahihi kibiblia?

Yeremiah 5:1

- Ni watu wangapi Mungu alikuwa anatafuta?
- Nini kingetokea kama angempata mtu?

Ezekieli 22:30

- Ni watu wangapi Mungu alikuwa anatafuta?
- Nini kingetokea kama angempata mtu?
- Nini kingetokea kama asingempata mtu huyo?

Wakumbushe wanafunzi kwamba hata mtu mmoja anayemfuata Mungu kwa uaminifu anaweza kuokoa mji mzima kutoka kwenye uharibifu.

Kuwa mtu wa kuleta mabadiliko

Soma Luka 7:11-17

Hadithi inatokea Yesu na wanafunzi wake wanapokutana na mjane katika msiba wa mwanaye walipopita kwenye lango la mji. Wanafunzi wa Yesu wanapata msisimko kwa kuwa wameona muujiza. Mwanamke mjane na waombolezaji wanalia.

- Nini kimetokea katika hadithi hii?

Tumia kadi kutoka kwenye bunda la vionyeshi kupitia vitu hivi 8 tunaweza kujifunza kutoka kwenye hadithi hii kuhusu mtu anayeleta mabadiliko.

1. **Yesu alimwona.** Kulikuwa na watu wengi katika makutano. Wanafunzi wa Yesu walisisimka kutokana na muujiza waliokuwa wameuona. Lakini Yesu alimwona katikati ya makutano. Kama tunataka kuwa watu wa kuleta mabadiliko tunahitaji kuwa watu wanoona wengine. Tunahitaji kuhakikisha tunaona mtu mmoja mmoja, si kundi la watu.

2. "**Moyo wake ulimhurumia**." Kama tunataka kuleta mabadiliko,tunahitaji kuhisi huruma.
Tunahitaji kuwa watu ambao mioyo yao inavunjika tunapoona mahitaji ya wengine. Mara nyingi sana tunaacha kuona na kujali. Tunafanya nini tunapomwona mtu ambaye ni mhitaji katika jamii yetu? Tunafanya nini tunapomwona mwanamke ambaye mume wake ametelekeza familia babu/bibi akitunza watoto wadogo? Je tunahisi huruma?
Mwombe Mungu akupe upendo zaidi kwa jamii yako. Mwombe Mungu akufanye uone watu katika jamii yako kama anavyowaona.

3. **Alitoa maneno ya kutia moyo.** Mara nyingi watu wanahitaji mtu wa kuwajali na kuwatia moyo. Ni rahisi kufikiri tunahitaji rasilimali za kuwasaidia watu lakini mara nyingi wale wanaohitaji msaada hasa wanahitaji mtu wa kuwa karibu nao na kuwatia moyo.

4. **Yesu aligusa jeneza.** Yesu alipofanya hivi alifanya kitu ambacho kwa mila yake hakikuwa sahihi. Wayahudi waliamini ukigusa jeneza utakuwa usiye msafi. Yesu alikuwa tayari kuwa asiye msafi kumsaidia mtu. Tunahitaji kuwa tayari kujihatarisha kuwa wachafu kusaidia watu. Watu wanaweza kutuongelea au kutupinga lakini tunahitaji kufanya kile Mungu alichotuitia kufanya.

5. **Kuna nguvu katika neno la Mungu na maombi.** Yesu alipoomba mtu alifufuliwa kutoka kwa wafu. Kamwe usisahau kuomba katika hali unazokumbana nazo. Chukua muda kuwaombea watu. Fanya hivyo ukiamini Mungu kweli anaweza kubadilisha hali na anajali kuhusu aina zote za mahitaji. Wafundishe watu kusali ili waweze pia kujua nguvu ya Mungu.

6. **Kulikuwa na matokeo.** Kijana alifufuliwa kutoka kwa wafu. Lazima tuwe na matokeo kutoka kwenye kazi yetu. Kama unataka kusaidia, anza na vitu vidogo unavyoweza kufanya kwa urahisi. Ukishapata mafanikio watu watafurahi na watu wengi zaidi watakuwa tayari kushiriki. Mwishowe utaweza kufanya mambo magumu zaidi.

7. **Yesu alimrudisha mtoto kwa mama yake na akaondoka**. Mama alikuwa shujaa; aliongea. Alikuwa mtu muhimu. Tunaposaidia watu tunahitaji kuhakikisha hatujaribu kuchukua sifa na kufanya wote watuangalie. Acha mtu ang'are wanapowaambie wengine kilichotokea. Itajenga heshima yao kuliko wewe kuchukua sifa zote.

8. **Mungu alitukuzwa.** Mwishowe utukufu lazima urudi kwa Mungu. Daima hakikisha kwamba wakati kilakitu kikiwa kimekamilika Mungu ndiye anayepewa sifa.

Maelekezo: Pitia tena hadithi ya Mrs. Lee kutoka Moduli 1

Mrs. Lee ni mwanamke wa kweli anaishi Mekong. Anatamani sana kusaidia familia maskini katika jamii yake, hasa wale wasio na kazi. Alianza kutembelea baadhi ya familia kila mwezi akitafuta namna ya kuwasaidia waweze kuishi. Hapa ni hadithi tatu kati ya nyingi za jinsi alivyoweza kusaidia familia. Hadithi hizi ni za kweli.

Hadithi 1 – Mrs. Lee na bustani ya maua



Katika eneo lake, kulikuwa na familia maskini yenye watoto wawili. Wote mama na baba hawakuwa na ajira. Mrs. Lee alipita kuwatembelea na akaona kipande kidogo cha ardhi mbele ya nyumba yao. "Kwa nini msipande maua," aliuliza. "Mnaweza kufanya nyumba yenu kuonekana vizuri zaidi na pia kuyauza katika soko liliko jirani"

Mama katika familia hii alifanya hivyo, na akaanza kupeleka maua sokoni alikoyauza. Lakini muda si mrefu aligundua kwamba wanunuzi walikuwa wakiulizia aina nyingine pia za maua—lakini alikuwa na eneo dogo tu na hakuweza kupanda aina nyingine. Huyu mama, lakini, alianza kununua maua kutoka kwa wakulima wengine na kuyauza pamoja na ya kwake kwa faida. Sasa kwa kuwa alikuwa na nafasi ndogo sokoni ya kuuza maua yake, alifikiria moyoni mwake, " Naweza kuuza vitu vingine pia!" Sasa anaamka mapema kila asubuhi kununua ndizi na nazi na kuuza sokoni katika meza yake.

Hadithi 2 – Mrs. Lee na viazi vitamu



Familia nyingine iliyohitaji msaada ilitaka kufanya kazi lakini hawakujua cha kufanya na hawakuwa na ujuzi wowote. Walifanya kazi kama vibarua wa kilasiku lakini maranyingi hawakuweza kupata kazi. Mrs. Lee aliweza kuona kwamba familia hii walikuwa wachapa kazi na walitaka kufanya kazi hivyo alikwenda kutembelea familia nyingine kanisani ambao walikuwa wakulima wa viazi. Aliwauliza kama kilimo cha viazi vitamu kilikuwa na faida, kama kulikuwa na soko zuri, na mtu anahitaji nini kuanzisha kilimo cha viazi vitamu. Alipo jua kwamba ilikuwa kazi nzuri aliwaeleza familia kwamba Mungu ametuita kupenda jirani zetu na kuwatunza masikini na akawaomba kama wangekuwa tayari kufundisha familia maskini namna ya kuwa wakulima wa viazi vitamu. Wakakubali. Mrs. Lee akazitambulisha familia mbili. Ile familia maskini walifurahi sana kwamba sasa wangeweza kufanya kitu na haraka walienda na kukodi kipande kidogo cha ardhi na kila kitu ambacho kilikuwa cha lazima kuanza. Mwisho wa mwaka walikuwa na mavuno mazuri na waliweza kulipa kodi ya ardhi na pesa ya mbegu, nk, na bado wakabaki na faida nzuri kwa ajili yao.

Hadithi 3 – Mrs. Lee na upatanisho wa familia

Familia ya tatu Mrs. Lee aliyotaka kusaidia walikuwa wametengana na wazazi wao. Wazazi waliamini kwamba familia hii ilikuwa haifai na isingeweza kuwa chchote. Mrs. Lee alikutana na familia kujaribu kupatanisha sehemu mbili za familia hii. Mrs. Lee alitoa hakikisho kwamba angeitembelea familia ya watoto kila mara na kuwasaidia kuboresha maisha yao kama wazazi wangekuwa tayari kuwapokea na kuwasaidia kidogo. Matokeo yake wazazi waliamua kumwamini kijana wao na familia yake tena na kuwakopesha pesa ili waweze kuanzisha biashara ya vyuma chakavu.



Sasa kijana ananunua vitu vikuukuu vilivyotengenezwa kwa chuma na kuviuza tena dukani kwa ajili ya kuzungushwa tena. Sasa anaweza kuitunza familia yake shukrani kwa kile anachopata kilasiku na sasa anajihisi kama mtu mwenye hadhi.

KIKUNDI KIKUBWA CHA MAJADILIANO

- Ni kwa njia gani Mrs Lee analeta mabadiliko katika jamii yake?
- Umeshawahi kupata nafasi kuwa kama Mrs. Lee katika jamii yako? Umefanya nini?
- Ni kwa njia gani Mrs. Lee anafanya baadhi ya mambo yaliyotajwa katika somo la biblia la mama mjane?
    - *Anatazama watu. Alichagua familia na akaanza kuwatembelea.*
    - *Anawaonea huruma. Ana hamu ya kuwasaidia.*
    - *Anawatia moyo.*
    - *Anathubutu na yuko radhi kufanya kazi kwa bidii. Hawatii watu moyo tu bali anatafuta namna ya kuwasaidia.*
    - *Ingawa hadithi haisemi hili lakini tunaweza kuwa na uhakika kwamba aliomba.*
    - *Kulikuwa na matokeo.*
    - *Aliwaacha watu kuendelea. Wao, si yeye, ndio waliofanya kazi sokoni na kulima ardhi.*
    - *Mungu alitukuzwa. Haitajwi katika hadithi lakini baadhi ya watu waliongoka na kuwa wakristo.*
- Ni masomo gani tunayojifunza kutoka kwa Mrs. Lee?
    - Tunahitaji <u>kuwa na moyo wa kusaidia</u> na kuwa radhi kutoa muda wetu kufanya.
    - Tunahitaji kuchukua muda <u>kujenga mahusiano</u> na watu katika jamii yetu wanaohitaji msaada. Tunahitaji kuwatembelea kila mara kujenga imani na watu.
    - Tunahitaji <u>kuwasikiliza watu</u> – Watu wengi katika mazingira magumu wanataka kujisikia kama watu. Wajali na wapende. Kama wakijihisi kujaliwa basi wataweza kusikiliza ushauri zaidi. Tunahitaji kuhakikisha hatuna mwelekeo wa kuhukumu bali mwelekeo wa kutaka kusaidia. Kama watu wakihisi unawahukumu hawataelekea kukushirikisha.
    - Tunahitaji <u>kuleta mawazo</u> kusaidia watu waone namna mpya ya kufanya mambo. Mara nyingi watu hawajui kubadilisha Maisha yao. Maskini wanaweza mara nyingi kuhisi hawawezi kubadili hali yao na watakata tamaa kwa urahisi wanapojaribu kupata Maisha tofauti. Wanahitaji mtu ambaye yuko tayari kufanya kazi nao kuwapa mawazo kuhusu nini wanaweza kufanya kubadilisha Maisha yao.

- Tunahitaji kuwa tayari kufanya kazi kufanya mawazo yatokee. Mrs. Lee alinunua mbegu za mwanzo na kuanza kupanda na mwanamke. Hakumwambia tu cha kufanya. Alimtafuta mtu ambaye alikuwa tayari kuifundisha familia namna ya kupanda viazi vitamu na kuwasaidia kupata ardhi ambayo wangeitumia. Katika hadithi ya tatu alienda kwenye familia na kujadiliana nao. Hakuwaambia watu kitu cha kufanya tu; alihusika kwa vitendo katika kuwasaidia kuanza.
- Uwe tayari kuanza kidogo. Siyo kila mawazo yataleta madiliko wazi kama katika hadithi hii. Wakati mwingine tunahitaji kufanya hatua kwa hatua na siku kwa siku kusaidia. Usitegemee watu wote kufanya mabadiliko makubwa haraka. Wape hatua rahisi za mwanzo ambazo wataweza kuzikamilisha na kujiona wamefaulu. Wakisha faulu katika kitu kidogo watakuwa tayari zaidi kujaribu kitu kikubwa zaidi.

Kikundi cha kusaidia

Wakati mwingine ni vigumu kufikiria mawazo ya kusaidia watu. Namna moja ya kupata mawazo zaidi ni kuanzisha kikundi cha kusaidia. Hiki kinaweza kuwa kikundi cha watu ambao wanakutana mara moja kwa wiki kwa sababu wana nia ya kusaidia watu. Wanaweza kuomba kwa ajili ya kila kikundi wachosaidia na kushirikishana mawazo ambayo kwayo wanataka kusaidia kuleta mabadiliko.

Pamoja wataweza kupata mawazo zaidi ya ambavyo mtu mmoja angeweza. Usisahau kumwomba Mungu akupe hekima.

KATIKA VIKUNDI VIDOGO

Fikiria kuhusu picha ya familia kuanzia mwanzoni mwa somo. Fikiria namna ambavyo zinaweza kuwasaidia kubadilika kutoka kwenye hali waliyomo sasa na kuwa picha ya ambavyo Mungu anakusudia Maisha yao yawe.

Hitimisho

Zaburi 139:14-17.

Wakati mwingine ni rahisi kufikiri kwamba zamani yetu itatengeneza wakati wetu ujao. Kama tunazaliwa maskini daima tutakuwa maskini; kama wazazi wetu ni wakulima basi na sisi tutakuwa wakulima. Umeumbwa kipekee na Mungu akakupa karama na tabia ambavyo anataka uwe navyo na amekuweka katika familia alimotaka uzaliwe. Anataka utumie kile alichokupa kuleta mabadiliko. Kila mmoja wenu anaweza kuleta mabadiliko kwa hali yoyote anayokumbana nayo, iwe katika familia yako, na watu wengine, au kwa jamii yako. Mungu anaweza kukuita kuleta mabadiliko katika kanisa lako, jimbo lako au hata katika nchi yako.

Utumiaji

Waombe kikundi kutafakari na kuomba kuhusu maswali haya

- Maisha yako yakoje? Je unaamini Mungu anaweza kubadili Maisha yako ya siku za usoni? Omba ili Mungu aweze kukuonyesha namna ya kubadili Maisha yako ya siku za usoni.

- Chukua muda kufikiria mtu unayeweza kuanza kumsaidia. Ungependa kuwa sehemu ya kikundi cha kusaidia?

Kikundi baada ya kuwa wameishaomba, waombe wale ambao wanapenda kuunda kikundi cha kusaidia kukutana na wewe katika muda wa mapumziko. Wasaidie kugawanyika katika vikundi vya watu 4 – 8 na watie moyo kupanga lini watakutana. Waeleze katika mkutano wao wa kwanza wachague mtu wanayetaka kumsaidia. Anza kwa kutembelea watu hao. Waombeane ili Mungu awasaidie utakapowatembelea. Kwenye mkutano wa pili toa taarifa jinsi ziara ilivyokwenda na washirikishe maeneo yoyote ambayo ungehitaji mawazo kwa ajili ya namna ya kusaidia. Kama kikundi, mwombe Mungu akupe hekima na utumie ubunifu Mungu aliokujalia kufikiria njia zinazowezekana kusaidia. Kumbuka, usijaribu kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Chagua eneo dogo kuanza kusaidia.

Somo 4: Mungu ametupa mengi sana

Malengo:

1. Kutambua yote Mungu aliyotujalia
2. Kuelewa kwamba msaada wa ndani - wa kawaida na wa kiroho ni muhimu zaidi kuliko msaada wa kawaida – wa nje

Zana

1. Maandishi kwa ajili ya mchezo wa kuigiza
2. Mwongozo wa masomo ya Biblia kwa kikundi kidogo
3. Bunda la vionyeshi – Kadi za msaada

Utangulizi

Kabla ya darasa mwombe mtu mmoja ajiandae kusoma mazungumzo binafsi yafuatayo.

Muumini ana muda wa kuabudu na anasoma Mat. 25: 14-30. Kisha anasema ,

" Natamani ningekuwa kama mtumishi aliyepewa talanta tano ili niweze kufanya mambo makubwa kwa Mungu! Lakini nasikitika kwa ajili ya mtumishi aliyepewa talanta moja … Nadhani Bwana alikuwa mgumu muno kwake! ah, hainihusu kwa sababu sidhani kama mimi nina talanta yoyote au kipaji maalum kumtumikia Mungu na kumfanyia kazi! Isitoshe, Mimi ni maskini sana!!!! Ukweli wangu ni kwamba mimi siwezi kumsaidia mtu yeyote kwa sababau nina mahitaji mengi sana mimi mwenyewe . Ee Bwana, naomba unisaidie unipe talanta chache za kutumia …"

- Umeona nini kwenye igizo hili?
- Muumini maskini amesema nini?
- Je yuko sahihi kuhusu mawazo yake?
- Kwa nini alifikiria namna hiyo?

Somo la Biblia

KATIKA VIKUNDI VIDOGO

Soma Mathayo 25:14-30.

<u>Haya 16-18</u>

- Watumishi walifanya nini na talanta zao?
- Je unaweza kujifananisha na watumishi wanaotumia talanta zao au na mtumishi anayeificha?

Haya 19-23

- Bwana alifanya nini aliporudi?
- Alisema nini kwa wale walizidisha talanta zao?

Haya 24-28

- Nini lilikuwa tatizo la mtumishi aliyeficha talanta yake?
- Bwana alimwambia nini?
- Kwa nini unadhani waamini wengi hawatumii talanta zao?
- Tunaweza kufanya nini?

Kuondokana na visingizio vyetu

Maelekezo: Waombe wakujitolea 5. Mtake kila aliyejitolea asome kisingizio cha kawaida kimoja.

Mzee = "Oh, Natamani ningekuwa bado kijana. Ningekuwa na nguvu za kumtumikia Bwana kwa talanta zangu. Sasa mimi ni mzee sana na nimechoka."

Kijana = "Oh, natamani ningekuwa na umri mkubwa zaidi. Ningekuwa na ushawishi zaidi na ningeweza kuwaongoza watu kumtumikia Mungu kwa talanta zangu. Sasa ni vigumu sana, kwa sababu bado ni mdogo sana."

Mfanya biashara = "Oh, natamani ningekuwa na muda zaidi. Niko bize sana na kazi yangu kiasi kwamba sipati muda kabisa wa kusaidia wengine."

Mtu asiye msomi = "Oh, Natamani ningekuwa na elimu zaidi. Sijui chochote kuhusu Theolojia. Mchungaji pekee anaweza kuwasaidia wengine kwa sababu alienda shule ya Biblia na ana mafunzo."

Maskini = "Oh, Natamani ningekuwa na pesa zaidi. Ningemtumikia Bwana kweli. Sasa hivi mimi ni maskini muno kuweza kumsaidia mtoto yeyote tofauti na mimi."

MAJADILIANO KATIKA VIKUNDI VIDOGO

- Kipi kati ya visingizio hivi umewahi kutumia?
- Kipi kati ya visingizio hivi unasikia mara nyingi kutoka kwa watu wengi katika kanisa lako?
- Nini ilikuwa ni kisingizio cha mtumishi aliyeficha talanta yake?
- Je kisingizio hiki kilikuwa cha kukubalika kwa bwana wake?
- Je visingizio vyetu vinakubailka kwa Mungu?
- Tunaweza kufanya nini kushinda visingizio hivi?

Tunahitaji kuanza kuona yote Mungu aliyotujalia.

Mara nyingi tunasikiliza uwongo wa shetani na kuamini hatuna kitu chochote. Tunajilinganisha na wengine na tunaweza tu kuona kile tusichokuwanacho. Leo tutatazama tena kuona yote Mungu aliyotupa.

Kutusaidia tufikiri vizuri zaidi tutazingatia mambo matatu – Ya kawaida – ya ndani; Ya kawaida – Ya nje; Ya kiroho.

Ya kawaida – ya ndani humaanisha vipaji na uwezo ambavyo Mungu ametujalia. Kwa mfano: uwezo wa kuzungumza, uwezo wa kufanya maamuzi, uwezo wa kupika chakula, uwezo wa kuwasha moto…
Ya kawaida – ya nje humaanisha misaada yote ambayo Mungu ametoa katika jamii yako. Kwa mfano: maji, ardhi, jua, shule, nk.

Ya kiroho humaanisha vitu vyote tulivyo navyo kwa sababu ya uhusiano na Mungu. Kwa mfano: miujiza, sala, Nguvu ya Mungu, nk.

Hakikisha darasa linaelewa wazi tofauti kati ya makundi hayo matatu. Gawa darasa katika vikundi na waombe waanze kuchambua (Bunda la vionyeshi – Kadi za rasilimali) zinazotolewa kwa vitu walivyo navyo na wasivyonavyo katika jamii. Wakishamaliza waombe wafikirie vitu 5 zaidi walivyonavyo.

Waombe darasa watazame majibu yao yote. Waulize kama yupo yeyote asiye na chochote. Wakati ni rahisi kudhani hatuna chochote, ukweli ni kwamba Mungu ametubariki sana. Ametupa mengi sana.. Kuliko kufikiri kuhusu kile tusichokuwa nacho, tunahitaji kutumia kile Mungu alichotujalia.

Soma tena Mathayo 25:20-23.

- Nini kinatokea tunapotumia kile Mungu alichotujalia?
- Tunatumia vyote Mungu alivyotujalia?
- Tunawezaje kuwa bora zaidi katika kutumia vyote Mungu alivyotujalia?

Wakulima

Utafiti unaonyesha kwamba rasilimali tulizonazo ndani mwetu mara nyingi ni muhimu zaidi kuliko zile ambazo ziko nje yetu. Kama wakristu tunaelewa pia rasilmali za kiroho ni muhimu zaidi kwa sababu zinazidisha rasilmali zetu za kawaida.

Soma hadithi ifuatayo!!

Katika Constanza ardhi inarutuba. Kuna maji mengi na hali ya nchi ni nzuri kwa kilimo. Baada ya vita kuu ya pili ya dunia, wajapani waliokuwa wanakimbia magumu Japan baada ya vita walihamia eneo hili. Walipofika hawakuwa na chochote, nguo tu walizokuwa wamevaa. Waliishi kati wenyeji na kulima pamoja nao.

Baada ya miaka 20 wakulima wajapani waliishakuwa matajiri. Walikuwa na nyumba kubwa nzuri. Lakini, wakulima wenyeji walikuwa bado maskini na bado wanahangaika kulima angalau kitu cha kutosha kula.

Hii iliwezekanaje? Nini kilitokea? Walikuwa na rasilimali sawa za kimwili. Tofauti ilikuwa katika mawazo yao. Wajapani waliamini lazima daima ufanye kazi kwa bidii na kwamba kamwe usikate tamaa. Wakulima wenyeji waliamini Maisha yao kamwe yasingebadilika. Waliamini kwamba kwa kuwa baba zao na babu zao walikuwa maskini na wao wangekuwa maskini.

Mambo yalipokuwa magumu hawakufanya chochote kwasababu waliamini hiyo ndiyo ilikuwa hatima yao.

- Nini kimetokea katika hadithi hii?
- Ni namna gani ilikuwa muhimu jinsi watu walivyofikiri?
- Tunaweza kujifunza nini kutoka kwenye hadithi hii?
- Ni kitu gani kimoja tunatakiwa tukibadilishe kama matokeo ya hadithi hii?

Angalia*: Wasaidie darasa kuelewa kwamba ilikuwa ardhi ileile. Tofauti ilikuwa katika Imani na mawazo. Wajapani hawakuwa na rasilmali bora – za nje ila zilezile kama za wakulima wenyeji. Faidi wajapani waliyokuwa nayo ni kwamba walikuwa na rasimali bora – za ndani . Tunaweza pia kuwa na rasimali nzuri – za ndani kama tukitumia neno la Mungu kuathiri kufikiria kwetu na Imani zetu.*

Somo 5: Shetani ni Mwongo

Malengo

1. Shetani hudanganya hata katika kiwango cha msingi cha Imani kuhusu vitu kama kazi, matumaini, utu, uumbaji, nk—uwongo wake hutuweka kwenye umaskini
2. Kama wakristo tunahitaji kujua ukweli kwa maana ukweli utatuweka huru
3. Mungu ametuita kutumeisha mataifa, kitu ambacho pia ni pamoja na kuleta ukweli katika maeneo yote ya maisha

Zana

1. Bunda la vionyeshi — Kadi za uwongo

Utangulizi

Soma Yohana 8:44

- Haya hii inamwelezaje shetani?
- Nini mifano ya uwongo shetani anaweza kusema?
- Je uwongo wa shetani unatuathiri leo?

Shetani ni baba wa uwongo. Tangu mwanzo alidanganya na anaendelea kudanganya leo. Anataka tuwe maskini na wenye njaa. Anajua kama tukifuata sheria za Mungu tutabarikiwa na Mungu. Hataki hilo litokee hivyo anatuambia uwongo.

Ni uwongo wa aina gani shetani hutuambia?

Shetani hutudanganya kwa namna nyingi. Leo tutapitia tena baadhi ya uwongo anaosema unaoendele kutuweka maskini.

Pitia kila moja ya kadi za uwongo (Bunda la vionyeshi #5). Hakikisha darasa linaelewa uwongo. Waombe darasa wafikirie maneno ya uwongo mawili zaidi na kuyaongoza katika kadi tupu mbili.

Weka kadi sakafuni na waombe darasa waweke majani (maharage/njiti za meno) juu ya kila uwongo waliouamini au wanaouamini.

Ligawe darasa katika vikundi na uwaombe kujadili kila uwongo na kufikiri kuhusu nini ukweli wa Mungu katika uwongo huo. Watake kila kikundi kutoa ripoti.

Kazi ni laana na mzigo mzito. Ni vizuri kufanya kazi kidogo iwezekanavyo	Tumeumbwa kufanya kazi. Adamu alifanya kazi kabla ya anguko. Ni sehemu ya hadhi yetu na namna ya kumtukuza Mungu.
Tulizaliwa maskini na tutakufa maskini.	Mungu atatubariki kama tukiwa watiifu kwake.
Sisi ni maskini sana hatuhitaji kutoa. Watu wengine watupe.	Hata maskini kabisa hawasamehewi kutoa. Katika Malaki Mungu anawaambia watu hawabarikiwi kwa sababu hawamuweki Mungu kwanza. Anawaambia wamjaribu na waone kitachotokea kama wakianza kutoa kama alivyoamuru. Tunahitaji kutoa tukitambua kwamba Mungu ametupa kilakitu na yuko tayari kutupatia vyote tunavyohitaji.
Mungu anajali tu mambo ya kiroho. 	Mungu anajali hali zote za Maisha yetu. Mambo yote yaliharibika katika anguko na anataka kupatanisha hali zote za Maisha yetu na Yeye.
Mungu anatutaka tutangaze injili tu kwa jirani zetu —Hatuna haja ya kujali mahitaji yao ya kimwili.	Mungu ametuambia tumpende jirani yetu. Anapoeleza habari ya kondoo na mbuzi anatukumbusha kwamba upendo ni kutoa chakula, maji na malazi Alipoulizwa jirani yetu ni nani, anasimulia hadithi ya msamaria akikutana na mgeni aliyekuwa amejeruhiwa barabarani na akampa msaada wa matibabu.

Hatuwezi kubadilisha Maisha yetu bila msaada wa kifedha kutoka kwa mtu mwingine.	Mungu ameishatubariki tayari. Tunahitaji kufungua macho yetu na kuona yote Mungu aliyotujalia na kuanza kuyatumia. Tunapotumia kile Mungu alichotupa na kuwabariki wengine basi na yeye atatubariki. Katika sehemu ya 1 tuliongea kuhusu Mrs. Lee aliyewasaidia watu kwa kuwapa tu mawazo.
Baadhi ya watu ni bora kuliko watu wengine. Sisi si wa muhimu.	Sote tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu na Mungu anampenda kila mmoja wetu sana hata akamtuma mwanawe afe kwa ajili yetu. Hakuna watu wa juu wala wa chini katika ufalme wake. Amemuumba kila mmoja wetu kulingana na jinsi anavyotaka na ana mpango maalum na kila mtu.
Ujumbe wa injili unaathiri tu Maisha yetu ya kiroho.	Yesu alikufa ili kupatanisha maeneo yote ya Maisha, si mambo ya kiroho tu.

Nini matokeo ya uwongo huu?

Uwongo wa shetani unaweza kuwa na matokeo makubwa katika Maisha yetu.

Soma hadithi hii!!

Sehemu kubwa ya Israel ni jangwa. Hata hivyo kuna kitu cha pekee kuhusu jangwa hili. Baadhi ya sehemu za jangwa hili hazina mimea—sehemu hizo ni tupu na kavu sana. Sehemu nyingine za jangwa hili zina misitu. Sehemu hizo hutoa sana matunda na maua mengi sana kiasi kwamba yanauzwa kote duniani. Kwa nini kuna msitu karibu na jangwa? Watu wanaoishi kwenye maeneo ya jangwa ni waarabu. Wanaamini Allah amelaani ardhi. Hawafanyi chochote kwa sababu wanaamini kwamba ardhi si nzuri na kamwe haitakuwa nzuri. Watu wengine wanaoishi katika ardhi hii ni waisraeli. Wanaamini hii ni nchi ya ahadi aliyowapa Mungu. Wanaamini ni nchi inayotoa maziwa na asali kama ilivyoahidiwa katika Biblia. Wanaamini kwamba Biblia imetuambia kuitunzi ardhi na kuitawala na kuifanyia kazi. Kwa hiyo walitumia ubunifu wao kupata mawazo ya kutatua matatizo ya ukosefu wa maji. Walipata suluhu na kupanda msitu. Mungu alibariki jitihada zao na sasa wana zaidi ya wanachoweza kutumia.

- Kulikuwa na tofauti gani kati ya waarabu na wayahudi?
- Kulikuwa na tofauti gani katika ardhi ilichozalisha kati ardhi iliyomilikwa na waarabu na ardhi iliyomilikiwa na wayahudi?

Angalia*: Wasaidie darasa kuona kwamba waarabu waliamini uwongo wa shetani na matokeo yake ardhi yao haifai. Waisraeli waliamini ukweli wa Mungu na wanazalisha vingi kiasi cha kuuza vinavyozalishwa nje ya nchi.*

Angalia kila moja ya kadi za uwongo tena. Kwa kila uwongo mmoja fikiria tofauti kati mtu anayeamini uwongo huo na mtu anayeamini katika ukweli wa Mungu. Kwa mfano namba 1 – kazi ni laana. Kama mtu akiamini kwamba kazi ni laana hatafanya kazi kwa bii. Watamaliza kufanya kazi wakipata kiasi cha kutosha kula kwa siku hiyo. Hawatafurahia kufanya kazi na daima watatafuta namna ya kufanya kazi kidogo sana iwezekanavyo. Lakini kama wakiamini kwamba kazi ni sehemu ya hadhi yetu na namna ya kumtukuza Mungu basi watafanya kazi kwa bidi. Kwa sababu ya kazi yao nzuri wataweza kupata zaidi. Wana uwezekano wa kustahimili hata hali inapokuwa ngumu na hawatakata tamaa kwa urahisi

KATIKA VIKUNDI VIDOGO

Pitieni kila uwongo mmoja na jadili matokeo ya uwongo huo. Toeni taarifa kwa darasa.

Waombe darasa kupata picha ya jinsi jamii yao ingekuwa kama wangeamini ukweli na si uwongo. Jamii yako ingekuwa bora zaidi au mbaya zaidi? Je jamii yako ingekuwa zaidi kama Mungu anavyotaka iwe au pungufu?

Kama darasa, pata muda muombe kwamba Mungu avunje nguvu za uwongo katika eneo lenu na asaidie akili yenu ijazwe ukweli.

Tunaondoshaje uwongo?

Soma Yohana 8:31-32. *Kwa Wayahudi waliomwamini, Yesu alisema, "Kama mkiyashika mafundisho yangu mtakuwa wanafunzi wangu. [32] Kisha mtaujua ukweli, na ukweli utawaweka huru."*

- Tunajuaje Ukweli?
- Ukweli utafanya nini? (Utatuweka huru kutoka kwenye nini?)

Kama tunataka kuwa huru kutoka kwenye uwongo wa shetani basi tunahitaji ukweli utokao kwa Mungu. Mungu ameahidi kuwatumia wakristu “Roho wa kweli atakayetuongoza katika kweli yote” (Yohana16:13). Omba kwamba Mungu atakuonyesha ukweli na tumia muda wako kusoma Biblia kuelewa ukweli wa Mungu. Mwombe Mungu akusaidie kuelewa Biblia na kuelewa ukweli wake.

SOMO 6: Ukadiriaji wa mahitaji

Malengo

1. Kutoa taarifa kuhusu jamii.
2. Kusaidia kikundi kufikiria namna jamii yao inaweza kubadilika
3. Kusaidia kuanza kuweka mipango kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika jamii yao

Zana

1. Kadi tupu
2. Karatasi kubwa tupu

Utangulizi

Hatua inayofuata ya kuleta mabadiliko katika jamii yetu ni kuangalia jamii yetu kwa karibu na kuelewa bayana matatizo yetu ni nini na nini ni matumaini yetu kwa siku zijazo.

Chagua "noti ya dola/shilingi"—noti ya hela ndogo zaidi—kitu ambacho kila mmoja anakielewa.

Uliza kikundi kujibu maswali yafuatayo. (Tafadhali rekebisha maswali haya yaendane sarafu inayoeleweka zaidi kwa watu unaowafundisha.)

1. Mara ngapi namba 1000 zinatokea katika noti?
2. Mara ngapi maneno "elfu moja" yanatokea katika noti?
3. Iko wapi namba kwenye noti?
4. Rangi ya namba ni rangi gani?
5. Ni mnyama gani yuko nyuma ya noti?
6. Mnyama anafanya nini?
7. Watu wangapi wanaonekana nyuma ya noti
8. Ni maneno gani yanaonekana nyuma ya noti kwa juu
9. Nini rangi ya nembo upande wa kushoto nyuma ya noti?

Eleza kwamba wakati mwingine tuna mazoea na kitu ambacho hatukioni tena. Sababu ya mazoezi haya ni kutusaidia kuona jamii tena na kufikiria namna tunavyoweza kusaidia.

Familia

Chora maboksi matatu kwenye karatasi kubwa. Weka alama kwenye maboksi: maskini sana, maskini, tajiri. Katika kila boksi eleza ni familia yenye hali ya namna gani inafaa kuwa kwenye alama hiyo. Waulize kufikiria vitu kama

- Aina ya nyumba
- Chakula
- Mifugo
- Ardhi
- Mavazi
- Elimu
- Kazi

Wakishamaliza, uwaulize darasa kukadiria asilimia gani ya watu katika jamii yao wako katika kila moja ya maboksi matatu hayo.

Kwa mfano

Tajiri	Masikini	Masikini sana
Nyumba imara, mpunga wa ziada na nguo safi. Wana runinga (tv), pikipiki, DVD, ng'ombe, sofa. Kuna chakula cha kutosha kwa milo mitatu na nyama. Watoto hawana njaa wanapokwenda kusoma.	Wana nyumba tu, hakuna chochote ndani. Wana chakula cha kutosha kwa mlo mmoja tu kwa siku. Nguo chache tu. Wanakula majani ya viazi vitamu.	Nyumba inaanguka. Wanakula mlo mmoja kwa siku – wali na chumvi. Bila mboga.

Jamii

Wafanye washiriki wote wafanye kazi pamoja kutengeneza ramani ya Kijiji chao.

Kama unafundisha watu kutoka jamii zaidi ya moja, wagawe ili kila kikundi kitoke kwenye jamii moja. Kama kikundi kimoja kina watu zaidi ya sita kigawe katika vikundi viwili na kila kikundi kitengeneze ramani.

Baada ya ramani kukamilika, watake washiriki kuweka alama kwa vitu vifuatavyo:

a. Wapi watu hupata maji yao ya kunywa
b. Shule, hospitali, masoko, vituo vya afya, nk.
c. sehemu muhimu za kidini
d. sehemu watu wanakopata mafuta ya kupikia
e. Barabara muhimu, nk.
f. Sehemu za kupumzikia

RAMANI MFANO



Mara baada ya ramani kukamilika waambie walinganishe ramani zao kuona kipi ni tofauti na kipi ni kinafanana. Kama wanatoka kwenye jamii moja basi wanaweza kubadilishana mawazo kwa vitu ambavyo walivikosa.

Mara baada ya ramani hizi kukamilika, chora ramani ya pili inayoonyesha jinsi wanavyotaka jamii yao kuoneka miaka kumi kutoka sasa. Waulize kitu gani wameongeza kwenye ramani na kwa nini, na nini wamebadilisha. Ni kwa namna gani ramani hii ni tofauti na ramani ya kwanza? Andika kila mabadiliko ya msingi kwenye ukurasa wa mabadiliko ya msingi wa ripoti ya mafunzo.

Kupaumbelesha miradi

Fikiria mabadiliko ambayo ungependa kuona yakitokea katika familia. Andika kila moja katika kadi. Ongeza mabadiliko katika ramani za jamii na uyaandike katika kadi. Weka kadi zote pamoja. Omba darasa kazipitia na kuona kama kuna mabadiliko waliyotarajia kuona ambayo hayakuorodheshwa.

Waombe darasa kuzichambua na kuziweka katika mafungu: za Muhimu zaidi, za muhimu , na zisizo za muhimu. Kwa kadi ambazo ni za muhimu zaidi weka alama ya namba tatu kwenye kadi. Kwa kadi za muhimu weka alama ya namba mbili kwenye kadi. Kwa kadi ambazo si za muhimu weka alama ya namba moja kwenye kadi. Weka kadi pamoja tena na uliombe darasa kuzichambua tena kulingana na jinsi ilivyorahisi kwa tatizo kutatuliwa: Rahisi kutatua, hivyo hivyo, na vigumu sana kutatua. Kwenye ambazo ni rahisi kutatua weka alama namba 3, kadi ya hivyo hivyo alama namba 2 na kadi ya vigumu kutatua alama namba moja.

Pata kadi zote zenye alama 6 (au alama 5 kama hakuna kadi zenye alama 6) Hizi ni kadi ambazo ni muhimu zaidi na pia rahisi zaidi kupata. Kutoka kwenye kadi hizi chagua moja au mbili unazohitaji kuanza nazo.

Chukua muda kuomba na umwombe Mungu aendelee kukuongoza katika kazi yako. Kama muda ukiruhusu kihimize kikundi chako kuweka mipango kwa ajili kitendo cha upendo kinachofuata.

---

[i] Miller, Darrow, Bob Moffitt, and Scott Allen. (2005). Chapter 7: The ABCs of Culture. In The Worldview of the Kingdom of God (pp. 103-104). Seattle, WA: YWAM Publishing.

[ii] Miller, Darrow (2013) "13 Transforming Truths: A Bible Study for Community Flourishing" (p5) published by the Disciple Nations Alliance under the terms of the Creative Commons Attribution-ShareAlike 3.0 license.